TANGANYIKA FARMERS' ASSOCIATION PLC

TAARIFA YA WAKURUGENZI NA TAARIFA YA MAHESABU KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 OKTOBA 2021

YALIYOMO **UKURASA**

1.	Yaliyomo	1
2.	Ilani ya Mkutano Mkuu wa mwaka	2
3.	Taarifa Muhimu za Kampuni	3
4.	Taarifa ya Mwenyekiti	4
5.	Taarifa ya Wakurugenzi	7
6.	Tamko la Mkuu wa Idara ya Fedha/Mahesabu	14
7.	Taarifa ya Wakaguzi wa Mahesabu	15
8.	Taarifa ya Mapato na Matumizi	17
9.	Mizania	18
10.	Taarifa inayohusu Mtiririko wa Fedha	19
11.	Maelekezo kuhusu Mabadiliko kwenye Mtaji	20
12.	Maelezo juu ya Hesabu kwa Mwaka ulioishia tarehe 31/10/2021	21

ILANI YA MKUTANO MKUU WA MWAKA

ILANI INATOLEWA kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa wa Tanganyika Farmers' Association PLC utafanyika katika **viwanja vya TFA Arusha Shopping Centre vilivyopo barabara ya Sokoine, eneo la Ngarenaro, Mjini Arusha siku ya Jumamosi tarehe 05 Novemba 2022 mnamo saa nne asubuhi (04:00)** kwa madhumuni yafuatayo:-

1. Kufungua Mkutano Mkuu.
2. Kusoma Ilani ya kuitisha Mkutano Mkuu.
3. Kupitisha Ajenda za Mkutano Mkuu.
4. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika Mbeya tarehe 06/11/2021.
5. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika Mbeya tarehe 06/11/2021.
6. Taarifa ya Mwenyekiti.
7. Kupokea na kupitisha taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa Mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31/10/2021, pamoja na taarifa ya Bodi na Wakaguzi wa Nje wa Mahesabu.
8. Kupokea na kupitisha mapendekezo ya Bodi kuwa hakutakuwa na toleo la gawio kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31/10/2021.
9. Kuidhinisha malipo ya Wakurugenzi kwa mwaka unaofuata.
10. Mapendekezo ya kuuza magari chakavu ya Kampuni.
11. Kuthibitisha uteuzi wa Wakaguzi wa Nje wa Mahesabu na malipo yao.
12. Kufanya uchaguzi wa Wakurugenzi wa Bodi ya Tanganyika Farmers' Association PLC.
13. Shughuli nyingine yeyote ile pale ambapo taarifa inayostahiki itakuwa imepokelewa.
14. Kufunga Mkutano Mkuu.

Kwa Amri ya Bodi ya Wakurugenzi

Pendo Jacob
KATIBU WA KAMPUNI
13/10/2022

ELEZO:

- Nyaraka zote zinazohusiana na Mkutano Mkuu zinapatikana katika tovuti www.tfa.co.tz.
- Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye Matawi yote ya TFA na kwenye tovuti www.tfa.co.tz. Fomu ya Uwakilishi iliyojazwa inatakiwa kufikishwa/kutumwa katika ofisi za TFA Makao Makuu sio chini ya masaa 48 kabla ya Mkutano Mkuu, lasivyo fomu hiyo haitakubalika.
- Wanahisa wafike na kadi itakayowatambulisha kama kadi ya uanachama, cheti cha umiliki wa hisa, leseni ya udereva, kitambulisho cha mpiga kura, au kitambulisho cha taifa.

TAARIFA MUHIMU ZA KAMPUNI KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 OKTOBA 2021

Kampuni imesajiliwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya Makampuni (Sura ya 12 ya mwaka 2002).

SEHEMU KUU YA BIASHARA: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

OFISI KUU NA ILIYOSAJILIWA:	Barabara ya Zima Moto S. L. P 3010, Arusha. www.tfa.co.tz
BENKI:	NCBA (T) Limited Tawi la Arusha S. L. P 2715 **Arusha.**
	CRDB Bank PLC Tawi la Arusha P. O. Box 3150 **Arusha.**
MWANASHERIA WA KAMPUNI	Royal Attorneys Advocates & Legal Consultants S. L. P 2753 **Arusha**
KATIBU WA KAMPUNI:	Pendo Jacob S. L. P 3010 **Arusha.**
WAKAGUZI WA MAHESABU:	Ndamallya & Company, Certified Accountants, Authorised Auditors & Tax Consultants, S. L. P 340, **Arusha.**

TAARIFA YA MWENYEKITI

1. **UTANGULIZI**

Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa napenda kuwasilisha kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi taarifa ya mwaka wa fedha ulioishia 2020/2021 ikiwemo na hatima ya baadae ya TFA PLC kama inavyokusudiwa katika malengo makubwa.

Ni imani yangu kubwa kuwa Wanachama wetu wanayo kila sababu ya kupata huduma bora zaidi na kuona faida ya uwekezaji wao katika TFA PLC. Faida ya uwekezaji huo itakuwepo hasa pale kampuni yetu itakapokuwa inajiendesha kwa faida. Na sasa kampuni yetu imefanya faida kwa kipindi kilichopita kama inavyoonekana katika mahesabu yaliyowasilishwa kwetu.

Baada ya utangulizi huu mfupi na kwa heshima tena, naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2020/2021.

2. **UENDESHAJI WA BIASHARA TOKA 1/11/2020 - 31/10/2021**

Kampuni hii iliendelea na shughuli zake za kawaida katika kumhudumia mkulima kama ilivyo katika malengo yetu ya msingi. Taarifa hii ya uendeshaji wa shughuli za Kampuni imegawanyika katika idara zifuatazo:

2.1 IDARA YA BIASHARA - BIASHARA YA PEMBEJEO ZA KILIMO

Tunajivunia kutoa ripoti ya ukuaji wa biashara yetu ya pembejeo za kilimo kwa muda wa miaka saba mfululizo. Menejimenti yetu imechangia sana ukuaji wa biashara hii kwa kuzingatia na kutekeleza sera na maelekezo ya Bodi ya Wakurugenzi;

A. Tunajivunia kwamba, mauzo yetu yameongezeka kutoka TZS 6.9 Bilioni mpaka TZS 12.9 Bilioni. Ukuaji huu ni wa juu Zaidi kuwahi kurekodiwa katika kipindi kifupi kwa muda mrefu uliopita.
B. Ukuaji wa 87% wa mauzo umefikiwa kupitia timu ya Wakurugenzi, Menejimenti na ushirikiano thabiti wa wasambazaji.
C. Kampuni imeweza kutengeneza ushirikiano imara na watengenezaji na wasambazaji wakuu kutoka China, India, Kenya, Malaysia na Ufaransa.
D. Ushirikiano na Fertilux umeweza kukuza uagizaji wetu kutoka nje kutoka dola za kimarekani 500,000 mpaka dola za kimarekani 2,000,000. Pia tumeweza kutambulisha bidhaa mpya kwa ajili ya mbolea "TFA FAHARI" na tunakamilisha usajili wa bidhaa nyingine mbili.
E. Mipango na mikakati ya kuanza kununua nafaka na bidhaa nyingine kwa ajili ya kuuza nje ya nchi imeanza na tayari majadiliano yapo katika hatua za awali. Tunaamini tutafanikiwa kukamilisha majadiliano na kuanzisha mradi huu uliochelewa.

2.2 IDARA YA MAJENGO

Idara ya majengo imeendelea kuwa chanzo muhimu cha mapato mbadala baada ya idara ya biashara kwa TFA PLC. Idara ya majengo iliendelea kuwa imara licha ya kushuka kwa biashara ya kukodisha majengo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Idara ya majengo ilifanikiwa kupata wapangaji wapya na wakubwa katika eneo la TFA Arusha Shopping Centre ambao walifanya biashara yetu ya kukodisha majengo kuendelea kuwa imara zaidi.

Kuanzishwa kwa mfumo wa kielekroniki wa kuegesha magari kumesaidia TFA kurahisisha ufanyaji wa manunuzi kwa urahisi zaidi kwa wateja wetu na hatimaye kukuza biashara. Maegesho ya magari katika TFA Arusha Shopping Centre yamekuwa ni maegesho salama zaidi hapa mjini Arusha.

Kiwango cha upangishaji kimeongezeka hadi kufikia 93.2% baada ya miaka miwili ya Uviko-19 ambayo hapo awali ilishuka hadi 89.0%.

2.3 BIASHARA YA CHAKULA NA DAWA ZA MIFUGO

Tumeweza kukuza biashara yetu ya chakula na dawa za mifugo kwa kufungua duka la ziada Kateshi. Fursa katika biashara ya chakula na dawa za mifugo ni kubwa na tunaona kwamba, hatupaswi kuachwa nje ya biashara hii.

Tumeanza kusajili na kusambaza bidhaa za lishe bora za kuku, mbuzi, kondoo, nguruwe na mipango inaendelea ya kuanza kuuza bidhaa za wanyama wadogo.

Tumepokea bidhaa zetu za kwanza kutoka Malaysia kwa ushirikiano na kampuni ya Agrikima, ambayo inafanya vizuri sokoni.

Aina hii ya biashara imekuwa hadi kufikia biashara ya bilioni na tunakadiria ukuaji wa bilioni mbili katika miaka miwili ijayo kutoka sasa.

3. MIPANGO NA MWELEKEO WA TFA PLC 2021/2022

3.1 UTANGULIZI

Mwenendo wa biashara yetu kwa muda wa kipindi cha miaka saba tangu Bodi hii ya Wakurugenzi iwe madarakani na kusimamia shughuli zote zinazofanywa na Menejimenti ya TFA, kwa niaba yenu umekuwa wa mafanikio makubwa. Ni kwa kuzingatia haya tunapenda kuwasilisha kwenu, mipango ya usoni ya biashara yetu hii ya muda mfupi wa kati na mrefu. Niwaombe wanahisa wenzangu muendelee kutuunga mkono katika haya ili tuweze kufika kwa pamoja katika nchi ya "*asali na maziwa".*

Yafutayo ni Malengo na Mipango muhimu kwa TFA PLC siku zijazo:-

i. Tumeanzisha majadiliano na washirika wa ndani na nje ili kuendeleza kitengo chetu cha majengo. Tunaelewa kuwa uwekezaji katika majengo unayo changamoto kubwa ya kupata fedha na hivyo tumeanza hatua hizi ili kupata unafuu.

ii. Tumefanya mchanganuo wa mtindo wetu wa biashara na kujiridhisha kuwa, ni wakati mwafaka wa kuongeza biashara mpya hasa katika maeneo ya technolojia na bima. Haya yatatufanya imara siku za usoni (future business).

iii. Eneo jingine ambalo tunakusudia kulianzisha na kulikuza ni biashara ya nje. Tumemaliza kusajili mbolea "TFA FAHARI" na tumekusudia ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tutaweza kuanza kuuza bidhaa hii nchi za Zambia na Malawi.

iv. Juhudi za kujenga uwezo kwa timu yetu ya kiufundi ili kuweza kuuza bidhaa na kutoa suluhisho kwa wakulima zimeanza. Tumepeleka wafanyakazi wetu Nairobi Kenya kwa mafunzo na mwaka ujao tutawapeleka wafanyakazi Zaidi kwa ajili ya mafunzo. Hatua hii itatusaidia kubaki na ushindani kwenye soko.

v. Tumesaini mkataba na CARMATEC kwa madhumuni ya kukuza teknolojia ya kilimo na tunaamini kuwa, mwakani tutaweza kukuza teknolojia ya vijijini kwa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini Tanzania.

vi. Mipango bado iko mbioni kuanzisha na kusambaza kwa wakulima jarida lenye kuelimisha na kutoa mafunzo mbalimbali katika kilimo. Jarida hili litatolewa bure na litasheheni makala na taarifa mbalimbali za kilimo kote nchini.

4. **SHUKURANI**

Ninaomba kuchukua fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa niaba yangu binafsi, Wakurugenzi wenzangu pamoja na Menejimenti nzima kwa ushirikiano wenu ambao mmekuwa mkitupatia bila kuchoka.

Pia ninawashukuru Wanahisa (Wanachama) wote wa TFA PLC ambao wamekuwa wavumilivu kwa muda mrefu wakati kampuni yetu ikiwa inafanya hasara na sasa imeanza kufanya faida.

Kwa namna ya pekee ninaomba kuwashukuru wateja wetu ambao wamekuwa wakitumia huduma zetu mara kwa mara.

Mwisho na si kwa umuhimu ninaomba kuwashukuru wadau wengine wote ambao wamekuwa nasi katika biashara ambao ni pamoja na benki, watengenezaji na wasambazaji wa pembejeo, Serikali pamoja na taasisi zake na wengine wote ambao wamefanikisha TFA PLC kufika hapa ilipo leo.

Asanteni sana.



Peter E. Sirikwa
MWENYEKITI WA BODI

TAARIFA YA WAKURUGENZI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 OKTOBA 2021

Wakurugenzi wanawasilisha ripoti yao pamoja na taarifa ya mahesabu yaliyokaguliwa ya mwaka ulioishia tarehe 31 Oktoba, 2021.

USAJILI

Kampuni imesajiliwa nchini Tanzania chini ya sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002 kama kampuni ambayo ina wanahisa wengi na ina hati ya usajili nambari 1826.

DIRA PAMOJA NA DHAMIRA

Kusambaza bidhaa ambazo zina ubora wa hali ya juu pamoja na kutoa huduma yenye weledi kwa wateja wake wote; kuhakikisha kwamba wanachama wake wanapata faida kutokana na uwekezaji wao; kuwa muajiri ambaye ni chaguo la wengi na kuwawezesha wadau wake wote pamoja na jumuia kwa ujumla kupata maendeleo.

MAADILI YA MSINGI

Ili kutekeleza dira pamoja na dhamira ya TFA PLC Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Menejimenti inazingatia maadili ya misingi ifuatayo:

- Uaminifu na Uweledi
- Uwazi
- Uwajibikaji
- Kuzingatia na kutekeleza sera ya wajibu wa kijamii na
- Kuwajali wote ambao huduma na shughuli zetu zinawagusa kwa njia moja au nyingine

SHUGHULI KUU

Biashara ya kampuni ni uuzaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo yaani mbegu, mbolea, zana za kilimo, vifaa mbalimbali, viuatilifu na dawa nyinginezo za kilimo na ufugaji, pamoja na bidhaa ambazo zinashabihiana na bidhaa tajwa. Pia kukarabati majengo na kupangisha.

MIPANGO YA MAENDELEO YA SIKU ZA BAADAYE

Kampuni itaendelea kuongeza faida kwa kupanua wigo wa biashara yake na kuhakikisha uwepo wa bidhaa bora. Huduma kwa wateja wote zitaboreshwa kwa kuimarishwa na kipaumbele kitatolewa kwa bidhaa ambazo tayari zimeongezwa thamani. Kampuni itapanua wigo wa huduma zake kwa kuongeza bidhaa zake sokoni ikizingatia gharama kwa makini.

UTAWALA BORA WA KAMPUNI

Bodi ya Wakurugenzi inajumuisha Wakurugenzi sita (6) ambapo mmoja wao anashikilia wadhifa wa Mkurugenzi Mtendaji. Bodi ya Wakurugenzi inawajibika na shughuli zote za kampuni ikiwa ni pamoja na; kutambua na kuainisha maeneo yote ambayo yanaweza kuwa na athari kwenye utendaji pamoja na kwenye utekelezaji wa majukumu ya kampuni, kuchunguza na kufuatilia maamuzi yote ya kuwekeza, na kuhakiki masuala muhimu ya kifedha. Aidha ni jukumu la Wakurugenzi kutathmini utendaji wa kampuni kwa makini na kuhakiki uwekezaji wote ambao unafanywa na kampuni ikizingatia kwa makini masuala yote ya fedha. Pamoja na hayo yote, Bodi ya Wakurugenzi inalo jukumu la kutathmini utendaji wa kampuni kulingana na mpango mkakati wake.

Wakurugenzi wanao wajibu wa kuhakikisha kwamba kampuni ina mfumo thabiti wa ndani wa kusimamia utekelezaji wa sera na taratibu za matumizi yote ya kampuni kwa kuzingatia misingi ya utawala bora**.**

Bodi ya Wakurugenzi inaukaimu uongozi wa siku hadi siku wa shughuli zote za kampuni kwa Mkurugenzi Mtendaji ambaye husaidiwa na Menejimenti ya TFA PLC kwenye kutekeleza majukumu hayo. Menejimenti inalo jukumu la kuendesha shughuli zote za kampuni kwa weledi wa hali ya juu. Ni jukumu la Menejimenti kuhakikisha kwamba kampuni inazingatia kwa ukamilifu misingi yote ya utawala bora. Wakurugenzi wanatambua pamoja na kuelewa fika umuhimu wa uadilifu, uweledi, uwazi, pamoja na uwajibikaji.

MTAJI WA KAMPUNI

Mtaji wa kampuni ni hisa ambazo zina jumla ya thamani ya TZS 2.5 bilioni pamoja na akiba iliyopo hivi sasa.

MATOKEO YA BIASHARA PAMOJA NA GAWIO

Matokeo ya biashara yameainishwa kwenye ukurasa wa 17. Wakurugenzi hawapendekezi toleo la gawio kwa mwaka huu.

USIMAMIZI WA ATHARI ZINAZOWEZA KUJITOKEZA PAMOJA NA UTHIBITI WA NDANI

Bodi ya Wakurugenzi inawajibika na usimamizi wa athari zote ambazo zinaweza kuikabili kampuni pamoja na kuandaa na kuweka misingi bora ya uthibiti wa ndani. Menejimenti kwa upande wake ina jukumu la kuhakikisha kwamba kampuni inayo mipango mathubuti ya kusimamia athari hizo pamoja na kuchukua hatua stahiki za uthibiti wa ndani ili kuhakikisha kwamba: -

- Shughuli zote za kampuni zinaendeshwa kwa ufanisi wa hali ya juu;
- Mali zote zinalindwa kikamilifu;
- Shughuli zote zinaendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria;
- Taarifa za mahesabu ni sahihi na za kuaminika;

- Biashara ya kampuni na kuwa endelevu hata pale ambapo hali ya biashara kwa ujumla ina sua sua; na
- Tabia ya kuwajibika kwa wadau wote.

Umahiri wa sera zote za uthibiti wa ndani unategemea kwa kiwango kikubwa utendaji ambao unazingatia kwa kikamilifu taratibu na maadili ambayo yamewekwa. Siku zote kuna uwezekano wa baadhi ya wafanyakazi wa kampuni kukiuka masharti hayo muhimu. Ijapokuwa hakuna taratibu za uthibidi wa ndani ambazo zinaweza kuhakikisha kwamba taarifa ambazo siyo sahihi au hasara isiyo ya lazima, haitokei, mfumo wa taratibu za uthibiti wa ndani za TFA PLC zinaipa Bodi ya Wakurugenzi uhakika kwamba taratibu zilizopo zinafanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

KUKAIMU

Malengo ya kampuni yanabuniwa na kukubaliwa na Bodi ya Wakurgenzi ambayo huyakaimu malengo hayo kwa Menejimenti kwa utekelezaji. Kampuni inao muundo ambao uko wazi na unahakikisha kwamba viwango vya madaraka pamoja na idhini kwenye ngazi mbali mbali za uongozi vimewekwa wazi.

BAJETI

Kila mwaka Menejimenti hutayarisha bajeti za kina na hatimae bajeti hizo hujadiliwa, kukubaliwa na kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi. Bajeti za kila mwaka hutayarishwa kutokana na matakwa na matarajio ya mpango mkakati wa kampuni. Wafanyakazi wenye uwezo unaohitajika huajiriwa kutokana na utaratibu wa ajira pamoja na mfumo wa tathmini wa utendaji. Mfumo huo huainisha mahitaji ya elimu na mafunzo kwa wafanyakazi. Mafunzo hayo hutolewa kwa wafanyakazi ndani ya kampuni pamoja na kwenye taasisi nyinginezo nje ya kampuni na hivyo kuimarisha ujuzi pamoja na uwezo wa wafanyakazi wote wa kampuni.

UTHIBITI WA NDANI (INTERNAL AUDIT)

Kitengo cha uthibiti wa ndani kimeanzishwa tena kutokana na kukua na kupanuka kwa shughuli za kampuni. Kitengo hicho kina jukumu la kutathmini hatari zilizopo kwenye shughuli za kampuni na kuthibiti usimamiaji. Kitengo kinahakikisha kwamba mapendekezo ambayo yanawasilishwa kwa Menejimenti yanafanyiwa kazi na kutekelezwa kwa ukamilifu. Meneja Uthibiti wa Ndani (Manager Internal Audit) anawajibika kiutendaji kwa Mkurugenzi Mtendaji lakini taarifa zake huwasilishwa moja kwa moja kwenye Bodi ya Wakurugenzi.

HALI YA KIFEDHA

Bodi ya Wakurugenzi inathibitisha kwamba taratibu pamoja na miongozo yote ya kiuhasibu imefuatwa kwenye utayarishaji wa taarifa hizi za fedha ambazo zimetayarishwa kwa kuzingatia mfumo wa kihasibu unaozingatia kwamba kampuni itaendelea kuwepo (***going concern basis***) kwa muda mrefu. Bodi ya Wakurugenzi inaridhika kwamba Tanganyika Farmers' Association PLC inazo rasilimali za kutosha kuiwezesha kampuni kuendelea kuwepo kwa muda mrefu sana.

USTAWI WA WAFANYAKAZI

Uhusiano kati ya Menejimenti na Wafanyakazi

Uhusiano kati ya Menejimenti na wafanyakazi uliendelea kuwa mzuri kwa kipindi chote cha mwaka huu wa fedha wa 2019. Hakuna migogoro yoyote ile ya ajira na utumishi ambayo haijapatiwa ufumbuzi.

KAMPUNI NI MWAJIRI AMBAYE ANAZINGATIA SERA YA NAFASI ZA AJIRA SAWA KWA WOTE BILA UBAGUZI

Kampuni inatoa fursa sawa kwa wote kupata ajira bila ya ubaguzi wowote ule na inahakikisha kwamba ajira inatolewa kwa wale ambao wanastahili bila ya kutumia vigezo vya jinsia, hali ya ndoa, kabila, dini, pamoja na ulemavu ambao haumpunguzii mhusika uwezo wa kutekeleza majukumu yake ya kazi.

MISAADA YA KIFEDHA

Mikopo, malipo ya awali ya mishahara na misaada mingineyo ya kifedha inatolewa kwa wafanyakazi wa kudumu kwa kutegemea tathmini ya tatizo husika na uwezo wa kampuni kwa wakati husika.

MPANGO WA MASLAHI KWA WAFANYAKAZI

Kampuni inalipa michango kwenye mashirika ya hifadhi ya jamii kwa mujibu wa sheria. Michango hiyo inatambulika kama mpango wa maslahi kwa wafanyakazi. Wastani wa idadi ya wafanyakazi kwa mwaka huu ilikuwa ni wafanyakazi 63.

MAHUSIANO YA KIBIASHARA PAMOJA NA MALIPO KWA WATU WALIO KARIBU NA KAMPUNI

Malipo yote ambayo walilipwa watu wa karibu na kampuni ikiwa ni pamoja na malipo yote ambayo walilipwa Wakurugenzi, yameonyeshwa wazi kwenye elezo nambari 9 la mahesabu haya.

UWIANO WA JINSIA

Kampuni ni mwajiri ambaye anatoa fursa za ajira sawa kwa watu wote bila ubaguzi. Hivyo TFA PLC inatoa fursa sawa kwa wote kupata ajira bila ya ubaguzi wowote ule na inahakikisha kwamba ajira inatolewa kwa wale ambao wanastahili bila ya kutumia vigezo vya jinsia, hali ya ndoa, kabila, dini, pamoja na ulemavu ambao haupumpunguzii mhusika uwezo wa kutekeleza majukumu yake ya kazi.

MPANGO WA KUDHIBITI MAZINGIRA

Kampuni inatathmini kwa karibu athari ambazo shughuli zake zinaweza kusababisha kwenye mazingira hususani kwenye matumizi ya nishati, maji na uzalishaji taka. Kampuni inahakikisha kwamba inapunguza kwa kiasi kikubwa athari zozote zile kwa mazingira na kuhakikisha matumizi bora ya maeneo yake kwa kuzingatia kwamba taka zote zinatupwa ipasavyo.

TAMKO KUHUSU MAJUKUMU YA WAKURUGENZI KUHUSIANA NA MAHESABU HAYA

Kwa mujibu wa sheria za Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002, Wakurugenzi wanao wajibu wa kutayarisha taarifa za kifedha ambazo zinaonyesha hali halisi ya kampuni pamoja na matokeo ya biashara yake kila mwisho wa mwaka wa fedha. Vile vile Wakurugenzi wanao wajibu wa kuhakikisha kwamba kampuni inaweka na kutunza kumbukumbu sahihi za mahesabu ambazo zinaonyesha hali sahihi ya kifedha na kwamba taarifa hizo zinakidhi matakwa ya sheria hiyo. Aidha Wakurugenzi wanao wajibu wa kutunza na kulinda mali zote za kampuni.

Wakurugenzi wanawajibika kulinda mali zote za kampuni na hivyo inawalazimu kuchukua hatua madhubuti kukabiliana na ubadhirifu pamoja na ukiukwaji wa sheria na taratibu. Wakurugenzi wanalo jukumu la kutayarisha taarifa za fedha ambazo ni za ukweli na sahihi.

MENEJIMENTI

Menejimenti ya kampuni inaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji na imegawanywa kwenye idara zifuatazo:-

- Idara ya Uthibiti wa Ndani (Internal Audit Department);
- Idara ya Fedha (Finance Department);
- Idara ya Mauzo na Masoko (Sales and Marketing Department);
- Idara ya Majengo (Property Department);
- Idara ya masuala ya Kikampuni (Corporate Department).

WAKURUGENZI NA UMILIKI WAO WA HISA ZA

KAMPUNI Wakurugenzi

Wakurugenzi wafuatao walitumikia kampuni kutoka tarehe 1 Novemba 2018 hadi tarehe ya taarifa hii:

S/N	Jina	Wadhifa	Tarehe ya kuchaguliwa/ kuteuliwa	Uraia
1.	Bw. Peter E. Sirikwa	Mwenyekiti	30/4/2016	Mtanzania
2.	Bi. Cathy-Elizabeth S. Long'lway	Naibu Mwenyekiti	30/4/2016	Mtanzania
3.	Bw. Walter S. Maeda	Mjumbe	30/4/2016	Mtanzania
4.	Bw. George B. Lupembe	Mjumbe	30/4/2016	Mtanzania
5.	Bw. Stanley J. I. Mwanri	Mjumbe	30/4/2016	Mtanzania
6.	Bw. Justin M. Shirima	Mkurugenzi Mtendaji	03/1/2017	Mtanzania

Kwenye mwaka ambao tunauongelea Bodi ya Wakurugenzi ilifanya jumla ya mikutano tano (5).

UMILIKI WA HISA ZA KAMPUNI

Wakurugenzi wanamiliki hisa za kampuni kama ifuatavyo

S/N	Jina	Idadi ya hisa
1.	Bw. Peter E. Sirikwa	970
2.	Bi.Cathy-Elizabeth S. Long'lway	15
3.	Bw. Walter S. Maeda	5,270
4.	Bw. George B. Lupembe	50
5.	Bw. Stanley J. I. Mwanri	965

WAKAGUZI WA MAHESABU

M/s Ndamallya & Company Auditors waliteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 170 (1) cha sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002, nao wameonyesha nia yao ya kuendelea na kazi hiyo kwa mujibu wa kifungu cha 170(2) cha sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002.

Kwa Amri ya Bodi ya Wakurugenzi

----------	----------	----------
Peter E. Sirikwa	**Rogasian D. Kimaryo**	**Justin M. Shirima**
Mwenyekiti	**Meneja wa Fedha**	**Mkurugenzi Mtendaji**
28/04/2022	**28/04/2022**	**28/04/2022**

TAMKO LA MKUU WA IDARA YA FEDHA / MAHESABU WA TANGANYIKA FARMERS' ASSOCIATION PLC

Mimi, Rogasian Donasian Kimaryo, FCPA 273 ni mkuu wa Idara ya Fedha / Mahesabu wa Tanganyika Farmers' Association PLC, ninakubali jukumu langu la kuhakikisha kwamba taaraifa ya hali ya kifedha iliyoishia tarehe 31 Oktoba 2021 yaliandaliwa kwa kufuata taratibu pamoja na miongozo ya kiuhasibu na taratibu za kisheria.

Ninadhibitisha ya kwamba taarifa ya hali ya kifedha inatoa msimamo wa ukweli na usawa wa mtazamo wa Tanganyika Farmers' Association PLC wa tarehe husika.

Imesainiwa na: _____

Cheo: Meneja wa Fedha

Namba ya ushiriki ya NBAA: FCPA 273

Tarehe: 28/04/2022

TAARIFA YA WAKAGUZI WA MAHESABU

Kwa wanachama wa
TANGANYIKA FARMERS' ASSOCIATION PLC

Tumekagua mahesabu ya TANGANYIKA FARMERS' ASSOCIATION PLC ambayo yamejumuisha taarifa ya hali ya kifedha kama ilivyokuwa mnamo tarehe 31 Oktoba 2019, taarifa ya faida na hasara, taarifa ya mabadiliko kwenye mtaji, pamoja na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa kipindi hicho ambacho kilimalizika, na muhtasari wa mahesabu wa sera za kihesabu na maelezo mengineyo kama yalivyo ainishwa kwenye kurasa nambari 19 mpaka 34.

MAJUKUMU YA WAKURUGENZI KUHUSU TAARIFA ZA FEDHA

Ni jukumu la Bodi ya Wakurugenzi kutayarisha taarifa za fedha ambazo zinakidhi matakwa ya taratibu za kimataifa za utayarishaji wa mahesabu (***International Financial Reporting Standards***) na kuzingatia pia matakwa ya sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002. Majukumu haya yanajumuisha mambo muhimu yafuatayo; kubuni, kutayarisha na kusimamia uthibiti wa ndani wa kampuni, kutayarisha taarifa za kifedha ambazo zinaonyesha hali halisi na ya ukweli bila ya kuwa na mapungufu ambayo yanatokana na udanganyifu au makosa ya kibinadamu, kuchagua na kuzitumia vyema taratibu bora za kihasibu. Aidha Wakurugenzi wanapaswa kuhakikisha kwamba makadirio pamoja na makisio yao yana misingi thabiti.

MAJUKUMU YA MKAGUZI WA MAHESABU

Jukumu letu sisi kama Wakaguzi ni kutoa maoni yetu ya kitaalamu na kitaaluma kwenye mahesabu hayo kulingana na matokeo ya ukaguzi wetu. Tumefanya ukaguzi kwa kuzingatia taratibu za kimataifa za ukaguzi wa mahesabu ***(International Standards on Auditing***). Taratibu hizo zinatuhitaji kupangilia na kutekeleza ukaguzi wetu ili kwamba tuweze kujihakikishia usahihi wa hesabu hizo.

Ukaguzi unajumuisha uchunguzi wa kina pamoja na kuthibitisha na kupata ushahidi wa kuridhisha kuhusu usahihi wa hesabu hizo. Utaratibu ambao unatumika unaendana na matakwa ya mkaguzi husika ambaye anapaswa kuhakikisha kwamba mahesabu hayo hayana mapungufu au makosa ambayo yanatokana na udanganyifu au makosa ya kibinadamu. Mkaguzi anao wajibu wa kujihakikishia kwamba kampuni inazo sera thabiti za usimamizi wa ndani. Aidha mkaguzi hufanya ukaguzi wa kina wa makisio na makadirio yaliyofanywa na Wakurugenzi. Mkaguzi anapaswa aridhie utekelezaji wa sera muafaka za utunzaji wa hesabu za kampuni na kuelezewa bayana.

Tumeridhika kwamba tumepata ushahidi wa kutosha kuthibitisha maoni yetu ambayo tunayatoa.

MAONI YETU YASIYO NA SHAKA

Kwa maoni yetu, taarifa za fedha zinatoa sura ya ukweli na isiyopotosha jinsi hali ya kampuni ilivyokuwa tarehe 31 Oktoba 2021 pamoja na matokeo ya mtiririko wa fedha kwa mwaka husika kwa kulingana na matakwa ya taratibu za kimataifa za utayarishaji wa mahesabu (International Financial Reporting Standards). Aidha taarifa hizi za fedha zimezingatia matakwa ya sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002.

TAARIFA KUHUSU MAJUKUMU MENGINEO YA KISHERIA Uzingativu wa Sheria ya Manunuzi, 2011

Kwa kuzingatia majukumu yetu kwenye sheria za manunuzi na kwa kuzingatia taratibu na mwenendo wa kimanunuzi, tuliyopitia kwa mujibu wa ukaguzi huu, Kampuni ya TANGANYIKA FARMERS' ASSOCITION PLC imezingatia matakwa ya sheria za **Manunuzi ya Umma, Na. 7 ya mwaka 2011**, pamoja na kanuni zake za mwaka 2013 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016).

NDAMALLYA & COMPANY
P.O. BOX 340
Phone 250 6196
250 5047
ARUSHA
Authorised Accountants & Auditors

Elia Makata, ACPA(T)
2492 Managing Partner.
Ndamallya & Company,

Certified Accountants, Authorised Auditors & Tax Consultants,

P. O. Box 340,

Arusha.

Tarehe: 28/04/2022

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 OKTOBA 2021

MAPATO	ELEZO	2020/2021 TZS'000	2019/2020 TZS'000
Mauzo	**3.0**	**12,968,214**	**11,602,832**
Gharama ya Mauzo	**4.0**	(11,889,379)	(10,099,289)
Faida ghafi		**1,078,835**	**1,503,543**
Mapato mengineyo	**5.0**	2,322,777	2,069,599
Faida ya uendeshaji		**3,401,612**	**3,573,142**
Gharama za uendeshaji			
Gharama za utawala	**6.0**	(1,606,230)	(1,634,577)
Gharama za uuzaji na usambazaji	**7.0**	(529,307)	(517,401)
Jumla ya gharama		**(2,135,537)**	**(2,151,978)**
Faida/(hasara) ya uendeshaji		1,266,075	1,421,164
Gharama za masuala ya fedha	**8.0**	(753,868)	(1,050,454)
Uchakavu (Depreciation)		(238,712)	(250,255)
Faida ambayo ilipatikana kutokana na Shughuli za kampuni kwa ujumla		273,495	120,455
Mapato mengineyo ambayo yanaweza Kujumuishwa kwenye hesabu za mapato na matumizi		-	-
Mapato/(hasara) yasiyo ya kawaida			
Faida kwa mwaka huu		**273,495**	**120,455**

Peter E. Sirikwa	**Rogasian D. Kimaryo**	**Justin M. Shirima**
Mwenyekiti	**Meneja wa Fedha**	**Mkurugenzi Mtendaji**
28/04/2022	**28/04/2022**	**28/04/2022**

MIZANIA KAMA ILIVYOKUWA TAREHE 31 OKTOBA 2021

Rasilimali za kudumu	**ELEZO**	**31.10.2021 TZS'000**	**31. 10. 2020 TZS'000**
Majengo, mitambo na zana	9.0	39,537,597	37,364,327
Kodi ya pango iliyolipwa awali	12.0	10,940	5,593
Kuwekeza kwenye rasilimali fedha	11.0	5,000	5,000
Jumla ya rasilimali za kudumu		**39,553,537**	**37,374,920**
Rasilimali za muda			
Bidhaa zilizopo	13.0	2,972,298	3,547,518
Hesabu za kupokelewa	14.0	1,606,689	1,443,045
Kodi ya mapato	10.0	2,719,224	2,672,718
Fedha taslimu na baki benki	15.0	671,830	729,013
Jumla ya rasilimali za muda		**7,970,041**	**8,392,294**
Jumla ya rasilimali zote		**47,523,578**	**45,767,214**
MTAJI NA MADENI			
Mtaji wa hisa pamoja na akiba iliyopo			
Mtaji wa hisa	20.0	2,513,694	2,513,694
Akiba ya urekebishaji (Reservation Reserves)	28.0	14,050,556	11,787,556
Akiba	21.0	20,876,647	21,779,107
Jumla ya mtaji		37,440,897	36,080,357
Madeni ya muda mrefu			
Mikopo	19.0	7,167,619	5,372,188
Madeni ya muda mfupi			
Hesabu za biashara za kulipwa	18.0	1,737,696	1,758,176
Ovadrafti ya benki	16.0	1,177,289	2,556,493
Jumla ya madeni ya muda mfupi		**2,914,985**	**4,314,669**
Jumla ya madeni kwa ujumla		10,082,681	9,686,857
Jumla ya mtaji na madeni		**47,523,578**	**45,767,214**

Peter E. Sirikwa	**Rogasian D. Kimaryo**	**Justin M. Shirima**
Mwenyekiti	**Meneja wa Fedha**	**Mkurugenzi Mtendaji**
28/04/2022	**28/04/2022**	**28/04/2022**

MAELEZO KUHUSU MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 OKTOBA 2021

FEDHA ZILIZOPATIKANA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA KAMPUNI	**ELEZO**	**2020/2021 TZS'000**	**2019/2020 TZS'000**
Faida kabla ya kodi ya mapato		273,495	120.455
Marekebisho yasikuwa ya kifedha kwenye mtiririko wa kifedha			
-Mali ambayo imeharibika		238,712	250,255
-Marekebisho ya mwaka uliopita		(1,175,955)	1,581,107
Marekebisho ya uchakavu		-	-
Kiasi cha fedha kilichotokana na shughuli za biashara		**(663,748)**	**1,951,817**
Marekebisho kwenye mtaji wa biashara			
(Ongezeko)/Upungufu wa bidhaa		575,220	(1,492,784)
(Ongezeko)/Upungufu wa fedha za kupokelewa		(163,644)	(126,246)
Ongezeko/(Upungufu) wa kodi iliyolipwa kabla ya muda wake		(46,506)	(129,665)
Ongezeko/(Upungufu) wa fedha za kulipwa		(20,480)	(238,431)
Jumla ya mabadiliko		344,590	(1,987,126)
Marekebisho mengine, jumla ndogo		-	-
Jumla ya mtiririko kwenye shughuli za Kibiashara (A)		(319,158)	(35,309)
Shughuli za uwekezaji			
Kuongezwa kwa majengo na mitambo	9.0	(149,501)	(344,436)
Marekebisho ya mali za muda mrefu.		(2,262,404)	1,905,098
Akiba ya urekebishaji		2,263,000	(1,910,000)
Faida iliyotokana na kuuzwa kwa magari chakavu		-	-
Kodi ya Pango iliyolipwa awali		(5,347)	(12,353)
Jumla ya mtiririko kwenye shughuli za uwekezaji (B)		**(154,252)**	**(361,691)**
Shughuli za kifedha			
NCBA mkopo wa muda mrefu		1,795,431	(558,142)
Mkopo wa kununua bidhaa (Letter of credit)		-	-
NCBA overdrafti ya benki		(1,379,204)	1,338,889
Jumla ya fedha iliyopokelewa kutokana na ingizo la fedha (C)		416,227	780,747
JUMLA YA MTIRIRIKO WA FEDHA (A+ B+ C)		(57,183)	383,637
Kiasi cha fedha mwanzo wa mwaka		729,013	345,376
Kiasi cha fedha mwisho wa mwaka		**671,830**	**729,013**

Mahesabu haya yaliidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe **28/04/2022** na kusainiwa kwa niaba yao na:

----------	----------	----------
Peter E. Sirikwa	**Rogasian D. Kimaryo**	**Justin M. Shirima**
Mwenyekiti	**Meneja wa Fedha**	**Mkurugenzi Mtendaji**
28/04/2022	**28/04/2022**	**28/04/2022**

Maelezo ambayo yameambatana na taarifa hii ni sehemu ya taarifa hii.

MAELEZO KUHUSU MABADILIKO KWENYE MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 OKTOBA 2021

MAELEZO	Mtaji wa hisa TZS'000	Akiba ya urekebishaji TZS,000	Akiba TZS'000	Jumla mnamo 31.10.2021 TZS'000	Jumla mnamo 31.10.2020
Baki kufikia tarehe 01.11.2020 b/f	2,513,694	11,787,556	21,779,107	36,080,357	32,468,800
Urekebishwaji	-	2,263,000		2,263,000	1,910,000
Faida (Hasara) ya mwaka	-	-	273,495	273,495	120,455
Marekebisho yaliyofanyika mwaka uliopita	-	-	(1,175,955)	(1,175,955)	1,581,107
Baki hadi tarehe 31.10.2021	2,513,694	14,050,556	20,876,647	37,440,897	36,080,357

Mahesabu haya yaliidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe **28/04/2022** na kusianiwa kwa niaba yao na:

----------	----------	----------
Peter E. Sirikwa	**Rogasian D. Kimaryo**	**Justin M. Shirima**
Mwenyekiti	**Meneja wa Fedha**	**Mkurugenzi Mtendaji**
28/04/2022	**28/04/2022**	**28/04/2022**

Maelezo ambayo yameambatana na taarifa hii ni sehemu ya taarifa hii.

MAELEZO JUU YA HESABU ZA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 OKTOBA, 2021

MAELEZO

1. KWA UJUMLA

TANGANYIKA FARMERS' ASSOCIATION PLC ilianzishwa kwa nia na jukumu kubwa la kuuza na kusambaza pembejeo za kilimo pamoja na bidhaa nyinginezo ambazo zina shabihiana. Aidha jukumu lake lingine ni kukodisha majengo ya biashara. Anuani yake iliyosajiliwa ni;

Barabara ya Zima Moto, Arusha S. L. P. 3010, Arusha. www.tfa.co.tz

2. MSIMAMO WA UHASIBU

Mahesabu haya yametengenezwa kwa kuzingatia msingi wa bei uliolipwa (***historical cost basis***) ambapo bei imelipwa kwenye mauzo na manunuzi ya mali zozote zile huzingatiwa. Misingi muhimu ya uhasibu ambayo imetumika imeelezewa hapa chini.

2.1 TAARIFA KUHUSU KUZINGATIWA MATAKWA NA VIGEZO VYA KIUHASIBU

Mahesabu haya yametengenezwa kufuatana na mfumo wa kimataifa wa utayarishaji wa taarifa za fedha (***International Financial Reporting Standards).***

2.2 MISINGI MIKUU YA UHASIBU

(a) Kutambua mapato

Mapato ghafi yanajumuisha mapato halisi ambayo yamepatikana kutoka kwenye huduma ambazo zimetolewa na kampuni kwenye shughuli zake za kawaida. Mapato ghafi yanaonyeshwa baada ya kupunguza kodi ya ongezeko ya thamani (VAT), marejesho kwenye malipo yoyote, pamoja na punguzo la bei.

Mauzo ya huduma yanatambuliwa kwenye kipindi ambacho huduma husika imetolewa kwa kuzingatia kumalizika kwa huduma hiyo.

(b) Shughuli ambazo zinahusu fedha za kigeni

i. Fedha iliyotumika

Kwenye taarifa hizi thamani ya fedha ambayo imetumika ni fedha ya Tanzania ambayo ndio fedha inayotumiwa kwa shughuli za siku hadi siku za kampuni.

ii. Shughuli za kifedha

Kwenye shughuli za kifedha ambazo zilihusu fedha za kigeni, thamani ya fedha hizo za kigeni imebadilishwa ili kupata thamani ya fedha ya Tanzania kulingana na viwango vya ubadilishaji fedha za kigeni kwenye siku husika. Mali pamoja na madeni yaliyopo kwenye thamani ya fedha za kigeni yameonyeshwa kwa thamani ya shilingi ya Tanzania. Hasara au faida iliyotokana na ubadilishwaji wa fedha hizo za kigeni umeoneshwa kama faida au hasara kwenye "Taarifa ya Mapato".

Taarifa na mahesabu haya yametayarishwa kwa thamani ya fedha ya Kitanzania (TZS'000), ambayo ndio sarafu inayotumiwa na kampuni.

Thamani ya kubadisha fedha za kigeni iliyotumika tarehe 31 Oktoba, 2021 ilikuwa:

1USD =TZS 2,296

(c) Gharama za malipo ya pensheni

Wajibu wa kampuni kulipa michango kwenye mpango wowote ule wa pensheni pamoja na mafao ya uzeeni, unaonyeshwa kwenye mahesabu haya kama gharama za kampuni. Malipo ambayo yanafanywa na kampuni kwenye NSSF kwa mujibu wa sheria pia yameonyeshwa kama gharama za kampuni.

(d) Kodi

Kodi imeonyeshwa kwenye mahesabu haya kama kodi ambayo imelipwa au kodi ambayo imehairishwa kulipwa na italipwa siku za usoni.

Kodi ya Kipindi kilichopo

Kodi ya kipindi kilichopo inajumuisha kodi ya mwaka huu pamoja na kodi yoyote ile ya vipindi vya nyuma ambayo inatarajiwa kulipwa kwa mamlaka husika - Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Viwango ambavyo vimetumika kukadiria kodi hiyo ni viwango vilivyopo kwa mujibu wa sheria. Kiwango cha hivi sasa ni 30%.

Kodi ambayo imeahirishwa kulipwa

Kodi ambayo imeahirishwa kulipwa imeonyeshwa kwenye mahesabu haya kwa ukamilifu.

Kodi ambayo imeahirishwa kwa muhtasari ni kodi ambayo kwa sababu moja au ingine bado haijalipwa. Kodi inaweza kuwa inatokana na sababu kadhaa ikiwemo sababu ya kampuni kuwa imepata hasara kwa miaka mingi.

(e) Mali, Majengo, Mitambo, Zana na Vifaa

Thamani ya mali, mitambo, zana na vifaa imeonyeshwa baada ya kupunguza uchakavu kutoka kwenye bei ya kununulia au kutoka kwenye thamani baada ya mali husika kutathiminiwa upya.

Thamani ya ardhi na majengo zinafutwa kwenye vitabu kwa utaratibu wa kutumia mstari ulionyooka (***straight line method***). Uchakavu wa mali nyinginezo za kudumu umefanywa kwa kupunguza thamani ya mali husika kila mwaka kwa kutumia viwango ambavyo vitapelekea kufutwa kwa thamani yote kwenye maisha ya mali hiyo (***reducing balance***).

kushuka kwa thamani kwa mali, mimea na vifaa vinahesabiwa kwenye usawa mstari wa moja kwa moja katika viwango vya kila mwaka.

Aina ya Mali	**%**
Ardhi na majengo	1.25
Magari makubwa	37.50
Magari madogo	25.00
Mashine na mitambo	12.50
Samani	12.50
Kompyuta na vifaa vyake	37.50

Viwango vya uchakavu vinavyotumika hivi sasa ni kama ifuatavyo:

(f) Mali ambazo zimepoteza thamani

Mali zote za kampuni tofauti na orodha na hasara iliyoahirishwa zimepitiwa kwenye kurasa yake ya kihesabu na kuonyeshwa mapungufu yake.

(g) Bidhaa za biashara

Thamani ya bidhaa za biashara imepatikana baada ya kufananisha na kuchukua bei ya chini kati ya bei ya kununulia na bei ambayo bidhaa hizo zinaweza kuuzwa kwenye hali ya kawaida ya soko/biashara kwa hivi sasa na kupunguza uchakavu.

(h) Madai ya biashara

Madai ya biashara yameonyeshwa kwa kiwango cha bei ya mauzo bila ya kuongeza riba yoyote ile. Thamani ya madai ambayo ulipwaji wake ni wa mashaka imezingatiwa. Madai yasiyolipika kabisa hufutwa kwenye vitabu pindi inapothibitika hivyo.

(i) Fedha taslimu

Kwenye "Taarifa inayohusu mtiririko wa fedha", fedha taslimu na mali nyinginezo ambazo ziko sawa na fedha taslimu, zimejumuishwa kwenye fedha taslimu zilizopo

mkononi, pamoja na fedha taslimu zilizopo kwenye mabenki.

(j) Kutengwa kwa viwango maalumu

Inapojitokeza kwamba kampuni ina wajibu kwa hivi sasa wa kulipa kiasi fulani kutokana na masuala yaliyotokea siku za nyuma, na kiwango cha malipo hayo kinajulikana bayana, basi kwenye mahesabu hayo kiwango cha kutosheleza kufanya malipo hayo kimetengwa.

(k) Madeni ya biashara na mengineyo

Mali na bidhaa ambazo bado hazijalipiwa (pale ambapo kampuni imekwisha kupokea hati ya madai ama laa) imeonyeshwa kwa bei halisi ya ununuzi bila ya kujumuisha riba yoyote ile.

(l) Hesabu kuhusu kodi ya pango iliyolipwa na kupokelewa awali

Kodi ya pango ambayo imepokelewa awali imeonyeshwa kwenye mahesabu ya faida na hasara kwa kuigawanya kodi hiyo kwenye kipindi chote husika cha upangaji.

MAELEZO JUU YA HESABU ZA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 OKTOBA 2019

		2020/2021	2019/2020
ELEZO 3.0	**MAPATO**	**TZS'000**	**TZS'000**
	Mauzo	**12,968,214**	**11,602,832**
	Mauzo yanatokana na mauzo ya pembejeo za kilimo.		
ELEZO 4.0	**GHARAMA YA MAUZO**		
	Bidhaa zilizokuwepo mwanzo wa mwaka	3,563,271	2,054,73
	Manunuzi ya mwaka huu	11,298,406	11,607,826
		14,861,677	13,646,807
	Bidhaa zilizokuwepo mwisho wa mwaka	(2,972,298)	(3,563,271)
	Jumla	**11,889,379**	**10,099,289**
ELEZO 5.0	**MAPATO MENGINEYO**		
	Kodi ya pango iliyopatikana	2,018,553	1,762,466
	Malipo ya kugharamia huduma (service charge)	191,241	225,704
	Jumuisho la mapato mengineyo madogo madogo	-	-
	Kamisheni	112,983	81,429
	Faida kutokana na mauzo ya magari chakavu ya kampuni	-	-
	Jumla	**2,322,777**	**2,069,599**
ELEZO 6.0	**GHARAMA ZA UTAWALA**		
	Kodi ya ujuzi na maendeleo (SDL)	33,332	38,311
	Gharama za fidia kwa wafanyakazi (WCF)	6,863	7,959
	Gharama za mafunzo kwa wafanyakazi	13,201	6,127
	Ada za Wakurugenzi	20,419	19,056
	Gharama za usafiri wa Wakurugenzi	55,989	81,432
	Gharama za mikutano ya Wakurugenzi	64,033	18,679
	Ada ya Uanachama kwenye Taasisi mbalimbali	15,270	3,041
	Ada za Ukaguzi	15,000	17,100
	Michango ya Hiyari	2,236	1,059
	Ustawi wa Wafanyakazi na gharama za matibabu	35,019	35,019
	Ushuru wa Stempu	40	-
	Magazeti na Vijarida	1,171	1,058

	Gharama za kufanya usafi	69,129	92,590
	Gharama za marekebisho na matengenezo	7,838	15,930
	Bima na Leseni	53,872	156,993
	Umeme	69,158	42,637
	Gharama za huduma za sheria	7,899	23,601
	Gharama za huduma za kitaalamu na kitaaluma	58,180	67,777
	Simu, usafirishaji barua na mawasiliano	27,871	34,335
	Kodi za viwanja na majengo	126,713	130,075
	Mishahara ya wafanyakazi	452,606	394,647
	NSSF	35,476	33,258
	Uchapishaji na steshenari	20,701	19,764
	Usafiri na usafirshaji	151,562	167,812
	Burudani	8,222	7,926
	Maji na uhifadhi	7,136	9,156
	Gharama za ulinzi	117,6231	136,561
	Gharama za kiinua mgongo	15,032	60,031
	Gharama za Mkutano Mkuu	77,244	12,630
	Uchakavu wa bidhaa	36,539	-
	Jumla	**1,606,230**	**1,634,577**
ELEZO 7.0	**GHARAMA ZA UUZAJI NA USAMBAZAJI**		
	Mishahara na Ujira	400,084	343,305
	Michango ya mwajiri NSSF	33,625	31,808
	Gharama za shukrani	-	-
	Matangazo na masoko	45,862	61,230
	Gharama za uendeshaji magari	49,736	81,058
	Jumla	**529,307**	**517,401**
ELEZO 8.0	**GHARAMA ZA MASUALA YA FEDHA**		
	Kamisheni na gharama za kibenki	17,072	87,661
	Riba ya benki	1,037,357	942,139
	Faida/Hasara za fedha za kigeni	(300,561)	21,305
	Jumla	**753,868**	**1,050,454**

ELEZO 9.0 MAJENGO, MITAMBO NA ZANA

MAJENGO, MITAMBO NA ZANA – 31 OKTOBA 2021

	Ardhi	Majengo	Mitambo, mashine na zana	Samani	Magari	Kompyuta na vifaa vyake	Jumla
	TZS'000	TZS'000	TZS'000	TZS'000	TZS'000	TZS'000	TZS'000
BEI/THAMANI							
Ilivyokuwa 1 Novemba 2020	23,122,000	15,478,544	139,201	161,905	323,622	239,245	39,464,517
Kuthaminisha kwa mara nyingine	3,308,000	(1,045,157)	-	-	-	-	
Ongezeko mwaka huu	-	102,714	6,544	1,004	10,801	28,438	149,501
Iliyouzwa	-	-	-	-	-	-	-
Ilivyokuwa 31 Oktoba 2021	**26,430,000**	**14,536,098**	**145,746**	**162,909**	**334,423**	**267,683**	**41,876,859**
KUSHUKA KWA THAMANI :							
Ilivyokuwa 01.11.2020	-	1,422,890	95,368	129,111	259,841	192,981	2,100,190
Kwa mwaka	-	181,561	6,297	4,195	18,646	28,013	238,712
Marekebisho ya uchakavu	-	1,604,451	101,665	133,306	278,487	220,994	2,339,262
Iliyouzwa		-	-	-	-	-	-
Thamani Halisi kwenye vitabu Hapo 31 Oktoba 2021	**26,430,000**	**12,931,647**	**44,081**	**29,603**	**55,936**	**50,715**	**39,537,597**
Hapo 31 Oktoba 2020	**23,122,000**	**14,055,654**	**43,833**	**32,794**	**63,781**	**46,264**	**37,364,327**

ELEZO 10.0 <u>GHARAMA ZA KODI YA MAPATO</u>

Mwaka huu hakuna kodi ya mapato kwani kampuni imelimbikiza hasara ya jumla ya TZS 2,672,718,000 kwa mwaka uliyoishia 2020.

Mchanganuo wa kodi kwa mwaka wa mapato 2020/2021

	TZS' 000	
Faida ya mwaka kabla ya kodi	273,495	
A: Jumlisha gharama		
zisizoweza kutolewa		
Michangoya hiari	2,236	
Ustawi wa wafanyakazi	29,908	
Burudani	8,222	
Jumla ndogo A		**313,861**

B: Kodi ya mapato ya kampuni 30%		
Toa kodi iliyolipwa awali		**94,158**
Ushuru wa muda uliolipwa		
Zuio la kodi ya majengo (10%)	(140,664)	
Jumla ya kodi iliyolipwa awali	-	
Kodi iliyokuwepo mwanzo wa maka	(2,672,718)	
(Tax brought forward)		**(2,813,382)**
Hasara ya kodi		**(2,719,224)**

ELEZO 11.O UWEKEZAJI KWENYE HISA ZA MAKAMPUNI	**31.10.2021 TZS'000**	**31.10.2020 TZS'000**
Happy sausages	5,000	5,000
Jumla	**5,000**	**5,000**

Kampuni ina hisa kwenye kampuni nyingine kama ambavyo imeonyeshwa hapo chini;

Jina la kampuni	**Idadi ya hisa**	**Idadi ya hisa**
Happy Sausages Ltd	**391**	**391**
Jumla ya hisa	**391**	**391**

ELEZO 12.0 KODI YA PANGO ILIYOLIPWA AWALI	**31.10.2021 TZS'000**	**31.12.2020 TZS'000**
Kodi iliyolipwa awali	**10,940**	**5,593**

ELEZO 13.0 BIDHAA	**2021 TZS'000**	**2020 TZS'000**
Bidhaa za kawaida	**3,011,953**	**3,563,271**
Punguzo; Thamani ya bidhaa zilizo Chakaa	**(39,655)**	**(15,753)**
Bidhaa zilizo njiani	-	-
Jumla	**2,972,298**	**3,547,518**

Gharama ya bidhaa ambazo zimeonekana kuwa ni gharama kwa kampuni kwa mwaka 2021 ni jumla ya TZS 11,889 bilioni (2020: TZS 10,099 bilioni). Gharama hii haijumuishi bidhaa ambazo zina jumla ya thamani ya TZS 39,655 milioni ambazo ni bidhaa zilizo chakaa. Bidhaa zinatarajia kuwa zimeuzwa ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili.

ELEZO 14.0 MAPATO YA BIASHARA PAMOJA NA MADENI AMBAYO KAMPUNI INATARAJIA

	31.10.2021 TZS'000	31.10,2020 TZS'000
Malipo yaliyopokelewa kutokana na kubadili fedha za kigeni	**1,532,549**	**1,296,184**
Malipo yaliyopokelewa yasiyotokana na kubadili fedha za kigeni	**74,140**	**146,861**
Jumla	**1,606,689**	**1,443,045**

ELEZO 15.0 FEDHA TASLIMU NA BAKI BENKI	**TZS'000**	**TZS'000**
Fedha taslimu	**8,997**	**3,494**
Baki Banki	**662,833**	**725,519**
Jumla	**671,830**	**729,013**

ELEZO 16.0 OVERDRAFTI YA BENKI	**TZS'000**	**TZS'000**
NCBA (T) Limited	**1,177,289**	**2,556,493**

Madhumuni ya ovadrafti hii ni kuhudumia biashara ya kampuni. Mkopo huu unatakiwa kulipwa wakati wowote ule ambapo benki itahitaji ulipwe vinginevyo utalipwa baada ya miezi kumi na mbili (12). Riba ambayo inatozwa ni asilimi kumi na sita (16%) kwa mwaka.

ELEZO 17.0 FEDHA TASLIMU NA BAKI BENKI

Kwenye mahesabu haya fedha taslimu mwisho wa kipindi husika ilikuwa ifuatavyo;

Fedha taslimu

	31.10.2021 TZS'000	31.10.2020 TZS'000
Fedha taslimu	**8,997**	**3,494**
Fedha iliyopo benki	**662,833**	**725,519**
Jumla	**671,830**	**729,013**

ELEZO 18.0 MADENI AMBAYO KAMPUNI INATAKIWA KUYALIPA KWENYE BIASHARA

	31.10.2021 TZS'000	31.10.2020 TZS'000
Madeni ya biashara	**1,657,560**	**1,673,472**
Madeni mengineyo	**80,136**	**84,704**
Jumla	**1,737,696**	**1,758,176**

ELEZO 19.0 MIKOPO AMBAYO INATOZWA RIBA

	TZS'000	TZS'000
Mkopo wa muda mrefu nambari I	5,781,129	5,224,735
(mkopo uliochanganywa)		
NCBA Fedha za mali (asset finance)	-	-
NCBA mkopo kwa ajili ya Bima	39,095	147,453
Mkopo wa matumizi wakati wa ununuzi wa bidhaa	-	-
Mkopo wa matumizi baada ya bidhaa kuwasili nchini	1,347,395	-
Jumla	**7,167,619**	**5,372,188**
Malipo ya kulipa ndani ya miezi	1,386,490	147,453
Kumi na mbili		
Malipo ya kulipa zaidi ya miezi	5,781,129	5,224,735
Kumi na mbili		
Jumla	**7,167,619**	**5,372,188**

NCBA MKOPO WA MUDA MREFU NAMBARI TZS

Madhumuni ya mkopo, ukomavu wake na riba inayotozwa

Madhumuni ya mkopo huu ni kuchanganya mikopo miwili (2) kuwa mmoja kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa TFA Shopping Centre. Mkopo huu utalipwa kwa awamu sitini (60) kwa riba ya asilimia kumi na sita kwa mwaka (16%).

Mkopo wa kununulia bidhaa za biashara

Madhumuni ya mkopo huu ni kuiwezesha TFA PLC kununua bidhaa nje na ndani ya nchi. Mkopo huu ni wa siku sitini (60) na siku tisini (90). Kwenye mkopo huu TFA inalipia kamisheni ya asilimia 0.75 kwa kila robo mwaka.

Dhamana zilizowekwa na TFA PLC kwenye mikopo mbali mbali

(a) Dhamana Namba. I

Tanganyika Farmers' Association PLC imeweka dhamana ya majengo yaliyopo kwenye majengo na nyumba kwenye Hati ya Kiwanja Na.055042/6 na 055026/1 kilichopo barabara ya Uhuru, maeneo ya Viwanda pamoja na barabara ya Babati ya Jiji la Arusha ambazo zote mbili zimesajiliwa kuwa na thamani ya soko ya TZS 30,650,000,000.00 (Shilingi za Kitanzania Bilioni Thelathini Mia Sita na Hamsini Millioni).

(b) Dhamana Nambari II

Tanganyika Farmers' Association PLC imeweka dhamana ya Majengo pamoja na nyumba zilizopo kwenye kiwanja Na.76, Kitalu 2E2, mtaa wa Boma jijini Arusha yenye Hati namba 055020/22, ambayo imesajiliwa kuwa na thamani ya soko ya TZS 3,777,000,000.00 (Shilingi za Kitanzania Bilioni Tatu Milioni Mia Saba na Sabini na Saba tu) kwajili ya kufidia mikopo na gharama zinginezo zinazohusiana kwa kiasi cha asilimia mia na ishirini na tano (125%).

(c) Dhamana Nambari III

Tanganyika Farmers' Association PLC imeweka dhamana ya Majengo pamoja na nyumba iliyo kwenye Kiwanja Na.100, Kitalu 'A', Sehemu I, barabara ya Boma iliyopo Manispaa ya Moshi, yenye nambari 12454-LR ambayo imesajiliwa kuwa na thamani ya soko ya TZS 1,650,000,000.00 (Shilingi za Kitanzania Bilioni Moja Mia Sita na Hamsini Milioni.)

(d) Dhamana Nambari IV

Tanganyika Farmers' Association PLC imeweka dhamana mali zote za kampuni ambazo zimesajiliwa kuwa na thamani ya soko ya TZS 10,350,765,000.00 (Shilingi Kitanzania Bilioni Kumi Milioni Mia Tatu Hamsini Laki Saba na Elfu Sitini na Tano tu) kwajili ya kufidia mikopo na gharama zinginezo zinazohusiana kwa kiasi cha asilimia mia na ishirini na tano (125%).

ELEZO 20.0 MTAJI WA HISA	**31.10.2021 TZS'000**	**31.10.2020 TZS'000**
Mtaji wa hisa ulio idhinishwa		
Hisa 300,000 za uanachama za Tzs 10,000 Kila mmoja	**3,000,000**	**3,000,000**
Uliotolewa na kulipwa		
Hisa 251,370 za uanachama za Tzs 10,000 Kila mmoja	**2,513,694**	**2,513,694**
Hisa ambazo bado hazijatolewa		
Hisa 48,630 za uanachama za Tzs 10,000 Kila mmoja	**486,306**	**486,306**

ELEZO 21.0 AKIBA	**31.10.2021 TZS'000**	**31.10.2020 TZS'000**
Baki iliyokuwepo mwanzo wa mwaka	21,779,107	20,077,550
Faida/(Hasara) kwenye mwaka huu	273,495	120,455
Marekebisho ambayo yamefanyika (Elezo 22)	(1,175,955)	1,581,107
Baki iliyopelekwa mbele	**20,876,647**	**21,779,107**

ELEZO 22.0 MAREKEBISHO YALIYOFANYWA MWAKA ULIOPITA

	TZS'000	TZS'000
Marekebisho ya vipindi vilivyopita yamesababishwa na kuzidishwa kwa hati ya madai ya wazuaji, kodi ambazo hazijalipwa, kutorekodiwa kwa za gharama za benki kwa mwaka uliyopita	(1,175,955)	1,581,107
Jumla	**(1,175,955)**	**1,581,107**

ELEZO 23.0 MIRADI MIKUBWA PAMOJA NA MADENI MAKUBWA YANAYOWEZA KUJITOKEZA

Hapakuwa na madeni yoyote makubwa yanaoweza kujitokeza wala mikataba ya miradi yoyote mikubwa ambayo ilikuwa imeidhinishwa mnamo tarehe 31 Oktoba 2021.

ELEZO 24.0 KUJILINDA NA ATHARI ZA KIFEDHA

a) Athari za kiwango cha riba

Kampuni imejilinda vyema na athari za kiwango cha riba kwani mikopo yote inaviwango vya riba ambavyo vimekubaliwa na kueleweka vyema na pande zote.

b) Athari za kutoa mikopo kwa wateja

Kwa kawaida kampuni huwa inaonekana kukabiliwa na athari ya kutoa mikopo kwa wateja kama kampuni inao wateja wengi waliopewa mikopo ya huduma au bidhaa hivyo kwamba wateja hao wasipolipa kwa wakati, hali ya kifeda ya kampuni husika itaathirika. TFA PLC ina wateja wachache sana kwenye majengo ya kupanga ambao wamepewa mikopo. Hivyo basi kampuni haikabiliwi na athari za kutoa mikopo.

c) Athari za fedha za kigeni

Wapangaji waliowengi wanatozwa kodi ya pango kwa kiwango cha dola za kimarekani. TFA PLC inakabiliana na athari za fedha za kigeni kwa kutumia fedha hizo zikiwa kwenye dola za Kimarekani kununulia bidhaa ndani pamoja na nje ya nchi.

d) Kujilinda na kushuka kwa ukwasi

TFA PLC inajikinga vyema na athari za kushuka kwa ukwasi. Kampuni hufanya hivyo kwa kuhakikisha kwamba ina baki ya kutosha, kukopa kutoka benki, nakuhakikisha kila mara kwamba inazo fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake.

ELEZO 25.0 WAFANYAKAZI

Kampuni ina wastani wa wafanyakazi 63.

ELEZO 26.0 KUSAJILIWA

Kampuni imesajliwa Tanzania kama kampuni binafsi chini ya sheria ya makampuni (Companies Act 2002) na ina usajili nambari 1826.

ELEZO 27.0 FEDHA

Taarifa hizi za fedha zimeonyeshwa kwa Shilingi za Kitanzania (TZS) kwani ndio sarafu ambayo kimsingi hutumika na kampuni. Aidha Katika shughuli zake kwa ujumla kampuni hutumia Shilingi za Kitanzania (TZS) pamoja na Dola za Kimarekani (US$).

ELEZO 28.0 AKIBA YA UREKEBISHAJI TZS 14,050,556

Mali za TFA PLC (Ardhi na Majengo) CT namba 055026/1, CT namba 055042/6 na ploti namba 76 bloku 'E' zilizoko Arusha na Ploti namba 100 bloku I '' A'' iliyoko Moshi ilithaminishwa kwa mara nyingine na

Business and Property Valuation Consultant (T) mwezi wa nane mwaka 2021na yafuatayo ni matokeo ya uthaminishwaji huo;

	TZS'000	**TZS'000**
Salio la kuanzia	11,787,556	9,877,556
Jumlisha: Ardhi	(1,045,000)	190,000
Majengo	3,308,000	1,720,000
Baki iliyopelekwa mbele	**14,050,556**	**11,787,556**

ELEZO 29.0 ULINGANIFU WA KIHESABU

Pale ambapo imekuwa ni lazima kufanya hivyo, tarakimu za mwaka uliopita zimerekebishwa ipasavyo kwa minajili ya tarakimu hizo kuwiana na mpangilio wa hesabu za mwaka huu.